East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 7, Issue 1, 2024
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

Original Article

Makosa ya Kiisimu Yanayofanywa na Wanafunzi Wanaozungumza Lahaja ya Kigichugu Wanapojifunza Kiswahili Kama Lugha ya Pili

Nancy Wanja Njagi[1*] *na David Kihara*[1]

[1] Chuo Kikuu cha Kenyatta, S. L. P. 43844-00100. Nairobi, Kenya.
[*] ORCID ID: https://orcid.org/0009-0003-4030-0841; Barua pepe ya mawasiliano: nancywanja127@gmail.com

DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1842

Tarehe ya Uchapishaji:

27 Machi 2024

Istilahi Muhimu:

Anafora, Harakia, Kanuni, Kisabiki, Sintaksia, Sintaksia Finyizi, Ufungami, Ukategoria, Utarakilishi, Utegemezi Muundo.

IKISIRI

Binadamu wanahitaji lugha ili kuwasiliana na mojawapo ya lugha maarufu ulimwenguni ni Kiswahili. Kiswahili kimetafitiwa na wataalamu wengi ili kutafuta suluhisho la baadhi ya changamoto zinazokumba lugha hii na kuiboresha. Mojawapo ya changamoto na suala ambalo halijatafitiwa na utafiti huu ulikusudia kubaini ni makosa ya kiisimu ya wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili : Uchunguzi kuhusiana na lahaja ya Kigichugu.Utafiti huu ulitumikiza kanuni na mihimili ya nadharia ya Sintaksia Finyizi ili kuweka wazi makosa ya kisintaksia na kisemantiki yanayofanywa na wanagenzi wa Kigichugu wanapojifunza Kiswahili kama L2. Uchunguzi huu uliendelezwa nyanjani na maktabani.Nyanjani ulitekelezwa katika shule za sekondari za kutwa katika kaunti ndogo ya Gichugu kwa sababu ndiko kuna wazungumzaji asilia wa Kigichugu. Katika utafiti huu tulipaswa kuteua shule,na wanafunzi wa kufanyia utafiti. Katika uchaguzi wa shule za kutwa za kufanyia utafiti tulitumia mbinu ya sampuli kimaksudi. Katika uteuzi wa wanafunzi tulitumia usampulishaji wa kinasibu pale ambapo tulipatia wanafunzi nambari kinasibu na kuteua waliopata nambari moja hadi sita. Data ya utafiti huu ilikusanywa kwa kutumia hojaji , insha na masimulizi . Data ya utafiti iliwasilishwa kupitia majedwali na maelezo. Matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha makosa mengi ya kisintaksia na kisemantiki yaliyotokana na lahaja ya Kigichugu. Makosa haya ni kama vile: makosa ya wanafunzi wagichugu katika matumizi ya nomino, vitenzi, vipatanishi, vivumishi, vibainishi, vielezi, vihusishi na vishamirishi. Makosa haya yalipelekea si tu kuibuka kwa muundo wa sentensi usiokubalika(sintaksia) bali hata kuwepo kwa maana, tofauti na iliyokusudiwa na wanafunzi hawa au isiyoeleweka, hivyo basi kuwepo kwa makosa ya kisemantiki (semantiki leksika na semantiki mantiki). Makosa haya yalichanganuliwa kwa kutumia nadharia ya Sintaksia Finyizi na kudhihirisha ukiukaji wa kanuni za nadharia hii.

APA CITATION

Njagi, N. W. & Kihara, D. (2024). Makosa ya Kiisimu Yanayofanywa na Wanafunzi Wanaozungumza Lahaja ya Kigichugu Wanapojifunza Kiswahili Kama Lugha ya Pili. *East African Journal of Swahili Studies*, *7*(1), 182-192. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1842.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1842

CHICAGO CITATION

Jafet, Janeth and Perida Mgecha. 2024. "Makosa ya Kiisimu Yanayofanywa na Wanafunzi Wanaozungumza Lahaja ya Kigichugu Wanapojifunza Kiswahili Kama Lugha ya Pili". *East African Journal of Swahili Studies* 7 (1), 182-192. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1842.

HARVARD CITATION

Njagi, N. W. & Kihara, D. (2024) "Makosa ya Kiisimu Yanayofanywa na Wanafunzi Wanaozungumza Lahaja ya Kigichugu Wanapojifunza Kiswahili Kama Lugha ya Pili", *East African Journal of Swahili Studies*, 7(1), pp. 182-192. doi: 10.37284/jammk.7.1.1842

IEEE CITATION

N. W. Njagi & D. Kihara "Makosa ya Kiisimu Yanayofanywa na Wanafunzi Wanaozungumza Lahaja ya Kigichugu Wanapojifunza Kiswahili Kama Lugha ya Pili", *EAJSS*, vol. 7, no. 1, pp. 182-192, Mar. 2024.

MLA CITATION

Njagi, Nancy Wanja & David Kihara. "Makosa ya Kiisimu Yanayofanywa na Wanafunzi Wanaozungumza Lahaja ya Kigichugu Wanapojifunza Kiswahili Kama Lugha ya Pili". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 7, no. 1, Mar. 2024, pp. 182-192, doi:10.37284/jammk.7.1.1842.

UTANGULIZI

Kiswahili kimekuwa muhimu sana nchini Kenya hasa katika kuendeleza mawasiliano , hivyo basi ni muhimu kuzungumza na kujifunza kutumia Kiswahili sanifu. Jambo hili hutatiza wengi hasa wanaojifunza Kiswahili kama L2. Martos (2023) anakiri haya na kusema kuwa, ujifunzaji wa lugha ya pili hutatiza watu wenye rasilimali na hata umri sawa kwani kuna vipengele vingine kando na umri ambavyo huathiri namna mtu anavyoimudu L2. Vipengele hivi ni : mitindo ya kujifunza , hamasa na mitazamo, mazingira ya kielimu , mazingira ya asili na lugha ya kwanza.Wengi wa wanafunzi Wagichugu hujifunza Kiswahili kama L2, hivyo basi, kimekubwa na athari za lahaja ya Kigichugu(L1). Hii ni kwa sababu wazazi wao ni Wagichugu na lugha ya wazazi wao ni Kigichugu. Hivyo basi, pana haja ya kuchunguza makosa ya kiisimu yanayohusiana na lahaja ya Kigichugu (L1) yanayotatiza jinsi wanavyoimudu lugha ya Kiswahili. Utafiti huu pia ulichochewa na kuwepo kwa dosari za kiisimu; kimofolojia, kisemantiki, na ya kisintaksia katika karatasi za mitihani (karatasi za sarufi na matumizi ya lugha; (102/2) na za insha (102/1) za baadhi ya wanafunzi Wagichugu wa shule za upili katika kaunti ndogo ya Kirinyaga Mashariki. Wengi wa wakaazi wa eneo hili ni Wagichugu na wengi wa watoto katika shule hizi hasa za kutwa ni Wagichugu ambao huzungumza lahaja ya Kigichugu kama lugha yao ya kwanza. Hivyo basi tulidhamiria kubaini makosa ya kiisimu yafanywayo na wanafunzi wanaozungumza lahaja ya Kigichugu wanapojifunza Kiswahili (L2).

MISINGI YA NADHARIA

Nadharia mbalimbali zimetumiwa kuongoza utafiti kuhusu makosa ya kiisimu yanayotokana na lugha ya kwanza katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Mathalani, Uchanganuzi Linganuzi, Uchanganuzi Makosa na Utabia. Utafiti huu ulitumia nadharia ambayo inaweza kueleza ujuzi wa kisarufi ili kueleza dhahiri makosa ya kisintaksia ambayo yanafanywa na wanafunzi Wakigichugu wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Mtazamo huu ni Sintaksia Finyizi.

Nadharia ya Sintaksia Finyizi iliasisiwa na Noam Chomsky mnamo miaka ya tisini (1995) kama marekebisho ya nadharia ya Utawala na ufungami iliyotokana na Noam Chomsky mwaka wa 1981. Nadharia za Sarufi bia ikiwemo Sintaksia Finyizi zilidhamiria kuboresha nadharia ya Sarufi Zalishi ambayo pia mwasisi wake ni Noam Chomsky. Nadharia hii ililenga kurahisisha uchanganuzi wa lugha yeyote ili iweze kueleweka na kufunzwa kwa urahisi (Chomsky, 2014). Noam Chomsky anaiwasilisha sio hasa kama nadharia bali taratibu ya kuichunguza lugha. Wanaisimu kadhaa pia wameiendeleza nadharia hii kama vile Liliane Haegeman (1995) , Lasnik (1993) na Marantz (1995). Nadharia hii ina mihimili kadhaa na kanuni ambazo zinarahisisha uchanganuzi wa sintaksia ya lugha tofauti. Mtazamo huu ni mwafaka katika utafiti huu kwa sababu uliweka wazi makosa ya kisintaksia ambayo wanafunzi

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1842

Wagichugu hufanya wanapojifunza Kiswahili kwa kuonyesha kanuni za kisintaksia wanazovunja wanapojifunza Kiswahili kama lugha ya pili.

Mihimili ya Nadharia ya Sintaksia Finyizi

Msingi mkuu wa mtazamo huu ni urahisishaji ambao hujitokeza kwa kutumia vifaa finyu, chache na vyepesi. Katika kuchanganua lugha kwa urahisi Chomsky (1995), alipendekeza vipengele vitatu vya uchanganuzi wa lugha vilivyotumika katika nadharia ya utawala na ufungami vitolewe.Vipengele hivi ni muundo wa ndani, nadharia ya X-baa na nadharia ya utawala. Nafasi ya muundo ndani ilichukuliwa na hatua za uchanganuzi wa kishazi. Hatua hizi ni muungano, uhamisho na idadisho.Vijinadharia hivi vilivyoondolewa, viligeuzwa na kuwa kanuni za kisintaksia ambazo tulitathimini katika utafiti wetu kwa kuchunguza zilivyokiukwa.

Mhimili mwingine wa nadharia hii ni kuwepo kwa kanuni za kisintaksia. Mwasisi wa nadharia hii (Noam Chomsky), alibomoa vijinadharia sita vya awali na akavitumia kama kanuni za sintaksia na ndizo zilizotumiwa katika uchanganuzi wa data ya utafiti huu. Ukiukaji wa kanuni hizi ambao tuliuangazia ndio hupelekea kuwepo kwa makosa ya kisintaksia. Kanuni hizi nimezieleza kwa undani katika ukurasa unaofuata.

Mhimili mwingine wa nadharia ya Sintaksia Finyizi ni ufasiri kamili. Kulingana na msingi huu elementi zote za sentensi zina jukumu maalum, aidha la kisemantiki, kifonolojia au kisintaksia (Mwihaki, 2007). Hivyo basi muundo wa sentensi yoyote lazima uwe na vipashio vilivyo na umuhimu. Kila kipashio katika sentensi basi lazima kiwe na maana mahususi. Tulitumia mhimili huu katika uchanganuzi wa data, pale ambapo tulitathimini maana ya maneno, semi, na nahau katika sentensi za wanafunzi Wagichugu ili kubaini makosa ya kisemantiki katika sentensi zile.

Kanuni ya iktisadi pia ni mhimili mwingine unaoeleza kuwa mifanyiko yote ya unyambuaji wa sentensi inapaswa kuwa na iktisadi. Yaani sentensi inapaswa kujumuisha vipashio vinavyotelekeza kazi fulani pekee.

Viwango vilivyo muhimu katika nadharia hii ni kijenzi fonetiki (PF) na kijenzi mantiki (LF). Viwango hivi ambavyo ni muhimu huunganishwa na mistari inayosimamia utarakilishi (computation). Hivyo basi kulingana na mhimili huu, viwango ambavyo ni nyeti vya lugha ni kile cha sauti na maana (Obuchi, 2010). Tulitumikiza msingi huu katika utafiti wetu pale ambapo tulichunguza mantiki ya sentensi za wanafunzi (maana) na pia makosa ya kifonetiki ambayo hupelekea kuwepo kwa ufasiri tofauti na uliokusudiwa.

Maneno

Kijenzi Fonetiki

Kijenzi Semantiki

Nadharia hii inaoanisha pia mofolojia na sintaksia. Inaeleza haipothesia ya ugawanyaji na uambishaji, suala linalohusiana na nyakati na ukubaliano. Nadharia ya Sintaksia Finyizi pia inaweka wazi kuwa ujumbe wa sentensi hubebwa na KT.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1842

Kanuni za Sintaksia Finyizi

Nadharia ya sintaksia finyizi ina kanuni saba; kanuni ya kwanza ni *kanuni leksia* ambayo hushikilia kuwa sifa za kileksia zinapaswa kufumana na jinsi sentensi ilivyoundwa na hazipaswi kuwakilishwa kando. Hii ni kwa sababu maana ya sentensi inategemea sifa za kileksia za maneno yalitotumika. Tuliitumikiza kanuni hii katika data ambayo tulipata pale ambapo tuliangazia ama mwanafunzi ametumia msamiati unaofaa, kwa sababu kutumia msamiati usiofaa huwa ni ukiukaji wa kanuni. Hivyo basi atakuwa amefanya makosa ya kisintaksia (Chomsky, 2014).

Kanuni nyingine ni *utegemezi muundo* ambayo inashikilia kuwa muundo wa sentensi hautegemei mfuatano wa maneno bali kategoria ya maneno. Vijenzi viwili vikifuatana, huwa vinazua ukuruba wa kisintaksia na iwapo ukuruba huu utakiukwa, makosa ya kisintaksia yatatokea (Newmeyer, 2021). Makosa haya hujitokeza mathalani, ukategoria unapopuuzwa hivyo basi, kusababisha mgongano wa vijenzi vya sentensi hiyo. Kwa kutumia kanuni ya utegemezi muundo, tuliangazia hasa ni vijenzi vipi ambavyo mwanafunzi anatumia mwanzoni na mwishoni. Kulingana na kanuni hii pia, sentensi huwa na kategoria tawala na ikidondoshwa makosa ya kisintaksia yanajitokeza kwani sentensi hufasirika visivyo, suala ambalo pia tuliangazia. Isitoshe kuna kategoria za maneno ambazo huhusiana kwa ukaribu, hivyo basi kusemakana kuwa vina unasaba, mathalani vitenzi na vielezi na uwakilishaji usiofaa wa kategoria hizi husababisha makosa ya kisintaksia, (Simile, 2022) suala ambalo pia tuliangazia katika uchanganuzi wa makosa ya kisintaksia. Makosa mengine ya kisintaksia yanayohusiana na kanuni hii, ambayo pia tuliangazia ni matumizi ya kategoria zaidi ya zinazohitajika katika sentensi.

Kuna pia *sheria ya uarifu* inayoshikilia kuwa kiarifu sharti kiwe na kiima (Mwihaki, 2007). Hivyo basi ili kuchunguza makosa ya kisintaksia yanayotokana na ukiukaji wa kanuni hii. Tuliangazia suala kama vile udondoshaji wa kiima katika sentensi za wanafunzi.

Pia kuna kanuni kuwa anafora lazima ifungamane na kisabiki ili maana ieleweke (*kanuni ya ufungami)*. (Mwihaki, 2007) Tulitumia kanuni hii ili kutathimini makosa ya kisintaksia kwa kujikita hasa kwa anafora na visabiki vya sentensi za wanafunzi. Tuliangazia, ni vipi mwanafunzi ametumia anafora isiyofaa? Kuna anafora katika sentensi zake? Na zaidi ya hayo, tuliangazia kisabiki kina nafasi gani kiharakia.

Isitoshe kuna *kanuni ya ufasiri kamili* ambayo hushikilia kuwa muundo wa kisemantiki lazima uwe kwa kijenzi cha sentensi,yaani lazima kiwe na maana ambayo ni moja tu (Chomsky, 2014). Haya, hasa huwa ni makosa ya kileksia ambayo hupelekea kuvunjwa kwa kanuni ya ufasiri kamili, mathalani matumizi ya istilahi isiyofaa katika sentensi. Licha ya hayo, kuna makosa ya tahajia mathalani unapodondosha sauti fulani, kuendeleza neno visivyo kwa kutenganisha neno linalostahili kuwa neno moja au kuunganisha maneno hivyo maana ya sentensi hiyo inakosa kueleweka. Makosa mengine yanayohusisha kanuni ya *ufasiri kamili*, ni kutumia nahau au msemo usio sahihi na kuvyaza kirai au neno kimakosa; mwanafunzi anahusisha matumizi ya neno katika muktadha wa awali kwa wa pili usiofaa. Hili hutokana na uzoefu wa matumizi yake katika muktadha wa awali.

MBINU ZA UTAFITI

Uchunguzi huu uliendelezwa nyanjani na maktabani.Nyanjani ulitekelezwa katika shule za sekondari za kutwa katika kaunti ndogo ya Gichugu kwa sababu ndiko kuna wazungumzaji asilia wa Kigichugu. Katika utafiti huu tulipaswa kuteua shule,na wanafunzi wa kufanyia utafiti. Katika uchaguzi wa shule za kutwa za kufanyia utafiti tulitumia mbinu ya sampuli kimaksudi pale ambapo tuliteua shule mbili za kutwa katika kila kata tukizingatia utendaji wao katika mtihani wa K.C.S.E wa Kiswahili. Tulichagua shule ya kwanza na ya mwisho katika kata hizo. Katika uteuzi wa wanafunzi tulitumia usampulishaji wa kinasibu pale ambapo tulipatia wanafunzi nambari kinasibu na kuteua waliopata nambari moja hadi sita. Data ya utafiti huu ilikusanywa

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1842

kwa kutumia hojaji , insha na masimulizi . Data ya utafiti iliwasilishwa kupitia majedwali na maelezo.

UCHANGANUZI WA MAKOSA YA KIISIMU

Sehemu hii ilichanganua makosa ya kiisimu ya wanafunzi wagichugu kulingana na kanuni za nadharia ya Sintaksia Finyizi. Nadharia ya Sintaksia Finyizi ina kanuni tano; kanuni leksia, utegemezi muundo, sheria ya uarifu, kanuni ya ufungami, na kanuni ya ufasiri kamili. Makosa haya yalichanganuliwa kwa utaratibu wa ukiukaji wa kanuni hizi za sintaksia finyizi na kutathimini usugu wa makosa ya kila kanuni iliyokiukwa.

Makosa ya Utegemezi Muundo

Kulingana na sheria ya utegemezi muundo, muundo wa sentensi hautegemei mfuatano wa maneno bali kategoria za maneno.Vijenzi viwili vikifuatana, huwa vinazua ukuruba wa kisintaksia na iwapo ukuruba huu utakiukwa makosa ya kisintaksia yatatokea (Adjer, 2003).Ukuruba huu utakiukwa iwapo ukategoria utapuuzwa, kategoria tawala itadondoshwa, unasaba wa vijenzi vya sentensi utapuuzwa au uziada wa kategoria utaongezwa katika sentensi. Makosa ya utegemezi muundo ya watafitiwa yalichanganuliwa kwa misingi hii minne.

Makosa ya Ukategoria Kupuuzwa

Ukategoria wa maneno unamaanisha aina ya neno katika muundo wa sentensi. Baadhi ya sentensi za wanafunzi Wagichugu zilisheheni makosa ya kupuuza aina za maneno zilizotumika katika sentensi, pale ambapo walitumia kategoria za maneno zilizofaa kuwa mwanzoni mwishoni na za mwishoni mwanzoni au katikati. Jedwali lifuatalo linabainisha haya.

Jedwali 1: Makosa ya Ukategoria Kupuuzwa

Kosa	Sahihi
Mbele ya garimoshi kulikuwa na mtoto mdogo.	Kulikuwa na mtoto mdogo mbele ya garimoshi.
Talanta zao walifanyisha kazi.	Walifanyisha kazi *talanta zao.*
Msitu ule *mwisho wake hungeona.*	*Hungeona mwisho* wa msitu ule.
Wanyama walionekana kuwa na *tabasamu moyoni.*	Tabasamu ilionekana *nyusoni* mwa wanyama.

Makosa ya Kupuuza Ukuruba wa Vijenzi

Ukuruba wa vijenzi vya sentensi unamaanisha uhusiano wa karibu wa viambajengo hivi unaovifanya kwa kawaida kufuatana katika muundo wa sentensi. Mathlani nomino zina unasaba wa kisintaksia na vivumishi navyo vitenzi vina ukuruba na vielezi. Sentensi zingine za wanafunzi Wagichugu zilikiuka kanuni hii, jambo lililosabisha sentensi zao kuvurugika. Jedwali lifuatalo linaonyesha baadhi ya makosa haya.

Jedwali 2: Makosa ya ukuruba wa vijenzi kupuuzwa

Kosa	Sahihi
Kabla ya mwalimu kuingia darasani nilimuona.	Nilimuona *kabla ya* mwalimu kuingia darasani.
Waziri wa afya alijaribu kupambana na *kubwa changamoto*.	Waziri wa afya alijaribu kupambana na *changamoto kubwa.*
Huu ugonjwa pia ulisababisha uhaba wa chakula.	*Ugonjwa huu* ulisababisha *pia* uhaba wa chakula.
Aliona *kazi yake ya bidii*.	Aliona *bidii ya kazi yake*.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1842

Katika lugha ya Kiswahili kitenzi aghalabu hutangulia kihusishi kwa sababu uamilifu wake huwa ni kutoa taarifa zaidi kuhusu kitenzi hicho. Hivyo basi kitenzi huwa na ukuruba wa kisintaksia na kihusishi. Si sahihi basi kusema 'kabla ya mwalimu kuingia darasani nilimuona'. Kitenzi 'nilimuona' kina unasaba wa kisintaksia na kihusishi 'kabla ya' na kinapaswa kukitangulia. Isitoshe, maneno 'bidii ya kazi yake' yana ukuruba wa kisintaksia kuliko 'kazi yake ya bidii.'

Makosa ya Uziada wa Kategoria

Kosa hili lilijitokeza pale ambapo wanafunzi walitumia kategoria zisizohitajika walipokuwa wakijaribu kusisitiza hoja. Jedwali lifuatalo linawakilisha haya

Jedwali 3: Makosa ya uziada wa kategoria

Kosa	Sahihi
Kuku *ile yao* **i**likufa.	Kuku *wao* alikufa.
Kila raia yeyote angepatikana bila barakoa alikuwa anapelekwa kwenye kituo cha polisi.	*Raia* yeyote angepatikana bila barakoa alikuwa anapelekwa kwenye kituo cha polisi.
Baadhi ya wengi walianza kazi ya kutapeli.	*Baadhi yao* walianza kazi ya kutapeli.
Mwisho wa hayo yote alimuaga.	Mwishowe alimuaga.

Jedwali hili linaonyesha wanafunzi walitumia kategoria za ziada zisizohitajika katika sentensi zao, mathalani, mwisho wa hayo yote badala ya mwishowe, kila raia yeyote badala ya raia yeyote, baadhi ya wengi badala ya baadhi yao.

Makosa ya Udondoshaji wa Kategoria Tawala

Watafitiwa wengine walidondosha kategoria tawala katika sentensi, jambo lilofanya maana iliyokusudiwa isijitokeze na mawasiliano yakatatizika. Jedwali lifuatalo litawakilisha makosa haya .

Jedwali 4: Makosa ya Udondoshaji wa Kategoria Tawala.

Kosa	Sahihi
Sherehe zile zilichukua wiki moja.	Sherehe zile zilichukua *muda* wa wiki moja.
Cha kwanza ni kukosa kushiriki katika uchimbaji wa kisima.	*Jambo* la kwanza ni kukosa kushiriki katika uchimbaji wa kisima.
Kila tulichotamani kula kilionekana kuwa kitamu.	Kila *chakula* tulichotamani kula kilionekana kuwa kitamu.

Kudondosha kategoria tawala, mathalani muda, jambo, na chakula katika sentensi zilizowakilishwa katika jedwali, kulifanya sentensi zile zifasirike vibaya. Mwanafunzi anaposema 'kila tulichotamani kula kilionekana kuwa kitamu' humpa msomaji fasiri pana kama vile labda anamaanisha matunda au chakula. Lakini unapotia kategoria husika(chakula) maana yake inafasirika vyema na kwa undani.

Usugu wa Makosa ya Utegemezi Muundo

Makosa ya utegemezi muundo yalibainika katika vitengo hivi vinne lakini kwa njia tofauti. Jedwali lifuatalo linaweka wazi jumla ya makosa katika kila kitengo.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1842

Jedwali 5: Makosa ya utegemezi muundo

Kigezo	Idadi	Asilimia
Udondoshaji wa kategoria tawala	28	48.2
Kupuuza unasaba wa vijenzi	8	13.8
Uziada wa Kategoria	7	12.1
Ukategoria kupuuzwa	15	25.9
Jumla	58	100

Kutokana na jedwali hii, ni dhahiri kuwa watafitiwa wengi waliofanya makosa ya utegemezi muundo walidondosha kategoria tawala (48.2%), wakifuatwa na waliopuuza ukategoria (25.9%), waliopuuza unasaba wa vijenzi (13.8%), na mwisho waliofanya makosa ya uziada wa kategoria (12.1%).

Makosa ya Uarifu

Kwa mujibu wa kanuni ya uarifu, katika muundo wa sentensi sahihi, kila kiarifu lazima kiwe na kiima. Makosa ya uarifu basi yalijitokeza pale ambapo sentensi za wanafunzi hazikuwa na kiima au kiima hakikuwa kimepatanishwa katika sentensi.

Jedwali 6: Makosa ya uarifu

Kosa	Sahihi
Cha kwanza ni kukosa kushiriki katika uchimbaji wa kisima.	*Jambo la kwanza* ni kukosa kushiriki katika uchimbaji wa kisima.
Alipokamilisha *hizo* alianza kuhutubia.	Alipomaliza *shughuli hizo* alianza kuwahutubia.
Walianza kufa kwa sababu ya njaa.	Wananchi walianza kufa kwa sababu ya njaa.

Makosa ya Ufungami

Kanuni ya ufungami hushikilia kuwa anafora lazima ifungamane na kisabiki ili maana ieleweke Radford (1997). Tulitumia kanuni hii kutathimini makosa ya kiisimu ya wanafunzi wagichugu kwa kujikita hasa kwa anafora na visabiki vya sentensi za wanafunzi. Radford (1997) alipendekeza vigezo vya ufangami ambavyo ni :

- Matumizi ya anafora inayofaa.
- Kuwepo kwa anafora zote katika sentensi.

Ukiukaji wa vigezo hivi hupelekea kuwepo kwa makosa ya ufungami na katika utafiti wetu baadhi ya wanafunzi Wagichugu walikiuka vigezo hivi. Tuligawanya makosa haya ya ufungami kwa vitengo hivi viwili kama ifuatavyo :

Makosa ya Wanafunzi Wagichugu ya Anafora Isiyofaa

Sentensi nyingi za watafitiwa zilisheheni makosa ya anafora isiyofaa kama inavyothibitishwa katika jedwali lifuatalo.

Jedwali 7: Makosa ya anafora isiyofaa

Kosa	Sahihi
Ugonjwa *huyu* uliangamiza watu wengi.	Ugonjwa *huu* uliangamiza watu wengi.
Kipepeo *ki*meruka.	Kipepeo *a*meruka.
*Ki*toto *k*ilianguka chini (ukubwa).	Toto *li*lianguka chini.
Samaki *i*livuliwa.	Samaki *a*livuliwa.
Kapaka *ka*lipotea jana (udogo).	Kipaka *ki*lipotea jana.
Jitu *a*liuliwa.	Jitu *li*liuliwa.
Makanisa *ya*lifungwa.	Kanisa *zi*lifungwa.
Maji *i*nayotiririka.	Maji *ya*nayotiririka.
Vitu *zinginezo.*	Vitu *vinginevyo.*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1842

Makosa mengi yaliyotokea ya anafora isiyofaa yalikuwa ni makosa ya ngeli na upatanisho wa kisarufi. Wanafunzi wengi walikosea katika uteuzi wa vipatanishi vya ngeli za nomino walizotumia katika sentensi zao. Matumizi ya anafora isiyofaa pia huenda yakasababishwa na kutomudu kwa wingi wa nomino hizo kwa baadhi ya wanafunzi. Makosa ya anafora isiyofaa yalijitokeza pia walipoandika udogo na ukubwa wa sentensi. Hili lilisababishwa na athari za lugha ya kwanza kwa sababu katika lahaja ya Kigichugu, kiambishi 'ki' hutumiwa kuashiria ukubwa na 'ka' udogo.

Makosa ya Wanafunzi Wagichugu ya Ukosefu wa Anafora

Baadhi ya makosa ya ukosefu wa anafora katika kazi za wanafunzi wagichugu yanabainika katika jedwali lifuatalo.

Jedwali 8: Makosa ya ukosefu wa anafora

Kosa	Sahihi
*Na*likuwa na watoto sita.	*Ni*likuwa na watoto sita.
Kukohoa kuliwa kumepigwa marufuku.	Kukohoa kuli*ku*wa kumepigwa marufuku.
Nafazi za kazi *kukosa.*	Nafasi za kazi *zili*kosa.
Wauguzi wengi *kupata* mda mgumu.	Wauguzi wengi *wali*pata muda mgumu.

Ni dhahiri kutokana na jedwali hili kuwa makosa ya ukosefu wa anafora yalijitokeza katika kazi za wanafunzi Wagichugu kama vile ukosefu wa vipatanishi vya nafsi, ngeli, na njeo. Mathalani katika sentensi; wauguzi wengi **kupata** muda mgumu badala ya wauguzi wengi **wali**pata muda mgumu ni kosa la ukosefu wa anafora, kwa sababu vijenzi *wa* na *li* katika **walipata** ambavyo ni vipatanishi va ngeli na nafsi mtawalia vinafaa kufungama kisabiki wauguzi. Makosa haya yaliathiri muundo wa sentensi na kuifanya ifasiriki isivyostahili.

Usugu wa Makosa ya Ufungami

Makosa ya ufungami yalibainika katika vitengo hivi viwili lakini kwa njia tofauti . Jedwali lifuatalo linaweka wazi jumla ya makosa katika kila kitengo.

Jedwali 9: Usugu wa Makosa ya Ufungami

Kigezo	Idadi	Asilimia
Anafora isiyofaa	97	90.7
Ukosefu wa anafora	10	9.3
Jumla	107	100

Kutokana na jedwali hii, ni dhahiri kuwa watafitiwa wengi waliofanya makosa ya ufungami walitumia anafora zisizofaa (90.7 %) kufungama visabiki katika sentensi zao. Asilimia ndogo (9.3%) walikuwa na makosa ya ukosefu wa anafora.

Makosa ya Ufasiri Kamili na Leksia

Kulingana na kanuni ya ufasiri kamili, muundo wa sentensi hauruhusu kuwepo kwa vijenzi ambavyo havitekelezi kazi ya kisemantiki. Isitoshe, vijenzi hivi vya sentensi vinapaswa kuwa na sifa zinazoafikiana na sifa za vijenzi vingine katika ile sentensi (Chomsky, 2014). Ukiushi wa haya hupelekea kuwepo kwa makosa ya ufasiri kamili. Vijenzi hivi huwa ni maneno (Leksia) na ikiwa maneno yale yameendelezwa vibaya, kazi ya kisemantiki ya yale maneno haitakuwepo, hivyo basi kutakuwa na makosa ya ufasiri kamili. Ukiushi wa kanuni leksia husababisha makosa ya ufasiri kamili. Sentensi za wanafunzi Wagichugu zilisheheni makosa haya ambayo tuligawanya katika vitengo vifuatavyo :

- Matumizi ya analojia ya dhana.
- Matumizi ya nahau isiyofaa.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1842

- Matumizi ya msamiati usiofaa.
- Matumizi ya tahajia isiyofaa.

Makosa haya yalikuwa ya kileksia lakini yalisababisha kosa la ufasiri kamili, kwa sababu vijenzi hivi vya sentensi havikuweka wazi kazi ya kisemantiki iliyokusudiwa.

Makosa ya Wanafunzi Wagichugu ya Tahajia

Jedwali lifuatalo linaakisi baadhi ya makosa ya tahajia ya wanafunzi wagichugu tuliopata katika utafiti wetu.

Jedwali 10: Makosa ya Tahajia

Kosa	Sahihi
Nafazi za kazi kukosa.	*Nafasi* za kazi kukosa.
Nilifika kabla ya *wazili* wa masomo.	Nilifika kabla ya *waziri* wa masomo.
Usafiri wa *madenge* yalifungwa.	Usafiri wa *ndege* ulifungwa.
Ng'ombe wetu amezaa *dama* mweusi.	Ng'ombe wetu amezaa *ndama* mweusi.
Kukidhi *maitaji* ya familia.	Kukidhi *mahitaji* ya familia.
Samaki *yundani* ya maji.	Samaki *yu ndani* ya maji.
Mtoto yule *ali kuwa* mtiifu.	Mtoto yule *alikuwa* mtiifu.
Aliamulisha kila mtu avae barakoa.	*Aliamrisha* kila mtu avae barakoa.
Mawaitha ya Profesa Mutahi Kagwe.	Mawaidha ya Profesa Mutahi kagwe.

Katika sentensi za wanafunzi Wagichugu kulikuwa na makosa ya tahajia kama vile kudondosha silabi au sauti ambazo ni sehemu ya neno, mathalani; maitaji, dama. Wengine walikosa kutenganisha maneno kama vile (yundani) badala ya (yu ndani). Maendelezo haya mabaya ya maneno yalisababisha ufasiri usiokusudiwa na mwanafunzi.

Makosa ya Analojia ya Dhana

Makosa ya analojia ya dhana hujitokeza pale ambapo mzungumzaji huhusisha muktadha wa awali wa matumizi ya neno kwa wa pili asiyozoea. Mathalani mwanafunzi aliona rahisi kutumia kihusishi 'na' ambacho hutumiwa katika lahaja ya Kigichugu kuonyesha kifaa kinachotumika kutekeleza kitendo cha kuchapa badala ya 'kwa' jambo lililoishia kuzua kosa. Makosa mengine yanayosababishwa na muktadha wa awali wa Kigichugu ni: kuja kwa mvua badala ya kunyesha, kugonga kengele badala ya kukiriza kengele na nambari ya wafanyikazi badala ya idadi ya wafanyikazi.

Jedwali 11: Makosa ya analojia ya dhana

Kosa	Sahihi
Hii ni kwa sababu *nambari ya* wafanyakazi ilipunguzwa.	Hii ni kwa sababu idadi ya wafanyakazi ilipunguzwa.
Tutaandaa shamba kabla ya *kuja kwa mvua.*	Tutaandaa shamba kabla ya *mvua kunyesha.*
*Aligonga k*engele.	*Alikiriza* kengele.
Nilichapwa *na* kiboko.	Nilichapwa *kwa* kiboko.

Makosa ya Wanafunzi Wagichugu ya Matumizi ya Nahau

Makosa haya yaliyoonyesha watafitiwa hawakuwa na umilisi wa kutumia misemo na nahau sanifu.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1842

Jedwali 12: Makosa katika matumizi ya nahau

Kosa	Sahihi
Kuweka bidii kazini.	*Kutia bidii* kazini.
Alitembea *kamwe kamwe* hadi nyumbani.	Alitembea *moja kwa moja h*adi nyumbani.
Alimwambia *afungue* masikio yake wazi.	Alimwambia *atege* masikio yake.

Makosa ya Wanafunzi Wagichugu ya Msamiati Usiofaa

Matumizi ya istilahi 'utumiaji' hayakufaa muundo wa sentensi ya kwanza. Msamiati sahihi na ambao ungefasirika vizuri katika sentensi hii ni 'matumizi'. Matumizi ya istilahi isiyofaa husababisha ukosefu wa mshikamano na maneno mengine katika sentensi na kuvuruga maana ya sentensi nzima.

Jedwali 13: Makosa ya msamiati usiofaa

Kosa	Sahihi
Utumiaji wa dawa za kulevya.	*Matumizi ya* dawa za kulevya.
Uongezekaji wa vifo.	Ongezeko la vifo.
Walioadhilika na ugonjwa huo.	*Waathiriwa* wa ugonjwa huo.
Watu *hawakuitikizwa* kutoka mijini.	Watu *hawakukubaliwa* kutoka mijini.

Usugu wa Makosa ya Ufasiri Kamili na Leksia

Jedwali lifuatalo linaakisi utokeaji wa makosa ya ufasiri kamili na leksia katika vitengo vyote vinne.

Jedwali 14: Usugu wa makosa ya ufasiri kamili na leksia

Makosa	Idadi	Asilimia
Analojia ya dhana	56	47.9
Msamiati usiofaa	17	14.5
Tahajia isiyofaa	40	34.2
Nahau isiyofaa	4	3.4
Jumla	117	100

Jedwali hili linaonyesha kuwa makosa ya analojia ya dhana (47.9 %) yalikuwa mengi yakilinganishwa na vitengo hivyo vingine; tahajia isiyofaa (34.2%), msamiati usiofaa (14.5 %) na nahau isiyofaa (3.4%). Makosa haya ya ufasiri kamili yalisababisha sentensi zifasirike tofauti na ilivyokusudiwa, hivyo basi hazikutekeleza kazi ya kisemantiki.

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Utafiti huu ulikuwa unabaini makosa ya kiisimu yafanywayo na wanafunzi wanaozungumza lahaja ya Kigichugu wanapojifunza Kiswahili (L2). Utafiti huu ulifanywa katika shule za upili za kutwa katika kaunti ndogo ya Kirinyaga Mashariki kwa sababu wengi wa wakaazi wa eneo hili ni Wagichugu na wengi wa watoto katika shule hizi hasa za kutwa ni Wagichugu ambao huzungumza lahaja ya Kigichugu kama lugha yao ya kwanza. Kutokana na matokeo ya utafiti , ni dhahiri kuwa lengo la utafiti huu liliweza kuafikiwa. Makosa ya kiisimu ya wanafunzi wagichugu kulingana na kanuni za nadharia ya Sintaksia Finyizi yaliweza kubainishwa. Wengi wa wanafunzi wagichugu walifanya makosa ya kiisimu katika insha zao, hojaji na masimulizi walioshiriki yaliyodhihirisha uvunjaji wa kanuni za nadharia ya Sintaksia Finyizi.

Utafiti huu haujajishughulisha na masuala yote ya lahaja ya Kigichugu na lugha ya Kiswahili. Tungependekeza basi utafiti zaidi katika ulinganishaji wa masuala ya kiisimu ya Kigichugu kama vile mifanyiko ya toni ya Kigichugu

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1842

ikilinganishwa na lugha ya Kiswahili,vishazi vya Kigichugu na virai vya Kigichugu.

MAREJELEO

Adjer, D. (2003). *Core Syntax: A Minimalist Approach.* London: Oxford University Press. https://doi.org/10.1515/tlir.2003.014

Chomsky, N. (1995). Categories and transformations. *The minimalist program*, 219, 394.

Chomsky, N. (2014). *The minimalist program.*(20th Anniversary ed.) MIT press.

Haegeman, L. (1995). *The syntax of negation (Vol. 75).* Cambridge University Press.

Lasnik, H. (1993). Case and expletives revisited: On Greed and other human failings. . *Linguistic inquiry*, 615-633.

Marantz, A. (1995). The minimalist program. Kwenye *The principles and parameters approach to linguistic theory* (kur. (pp. 351-382)). Blackwell.

Martos, P. L. (2023). *Anthropolojia ya Isimu: Mambo Yanayoathiri Mchakato wa Kujifunza Lugha Mpya*. Retrieved from YOAIR: https://www.yoair.com/sw/blog/linguistic-anthropology-factors-affecting-the-process-of-learning-a-new-language/

Mwihaki, A. (2007). Minimalist Approach to Kiswahili Syntax . *Kiswahili a referred journal*, 70, p. 27.

Newmeyer, F. J. (2021). Chomsky and Usage-Based Linguistics. *A Companion to Chomsky*, 287-304.

Obuchi, S. M. (2010). *Muundo wa Kiswahili: Ngazi na Vipengele.* Nairobi: A~Frame Publishers.

Radford, A. (1997). *Syntax: A Minimalist Introduction*.(1st edition) Cambridge: Cambridge University Press.

Simile, O. D. (2022). A Minimalist Approach to the Analysis of the Structure of the KɨbhwanƊi Determiner Phrase. *Journal of Linguistics & Language in Education*, 16(2).